# KISWAHILI KWA WAGENIMUHTASARI WA KUFUNDISHA NA KUJIFUNZA - NGAZI YA KWANZA

| Mada Kuu/Mada Ndogo | Malengo Mahususi | Sarufi | Msamiati | Njia za Kufundishia | Vifaa vya Kufundishia | Tathmini | Muda / Saa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salamu** | Kuweza kusalimia na kuitikia salamu mbalimbali kwa kuzingatia utamaduni wa Mtanzania | Nafsi ya 1, 2 na 3 (Umoja na Wingi) | Unaoendana na salamu na unaozingatia utamaduni wa Mtanzania katika hali mbalimbali<br><br>Semi mbalimbali | Mkufunzi atatumia mbinu ya mawasiliano kufundisha salamu mbalimbali za Kiswahili<br><br>Kila mshiriki na mwenzake wakiwa wawili wawili/katika vikundi watasalimiana katika mazingira tofauti<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuandika na kuzungumza<br><br>Mshiriki atafanya majaribio ya kusalimiana na wenyeji | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za video | Je, mshiriki ameweza kusalimia au kujibu salamu vizuri?<br><br>Je, amezingatia maadili na miiko ya kitamaduni wakati wa kusalimiana? | 4 |
| **Utambulisho** | Kuweza kujitambulisha na kutambulisha wengine kwa kuzingatia utamaduni wa Mtanzania | Viwakilishi nafsi<br><br>Vivumishi vimilikishi<br><br>Kitenzi *kuwa* Wakati uliopo Utaifa | Msamiati unaofaa na kulandana na utambulisho kwa kuzingatia umoja na wingi (nomino) | Mkufunzi atatumia mbinu na miundo mbalimbali kufundisha kujitambulisha na kuwatambulisha wengine<br><br>Mshiriki akiwa katika jozi atafanya mazoezi ya kujitambulisha<br><br>Washiriki wakiwa katika jozi | Picha, Majadiliano, Kanda za video, Kadi | Je, mshiriki ameweza kujitambulisha na kuwatambulisha wengine kwa usahihi?<br><br>Je, alizingatia maadili na miiko ya | 4 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | vitenzi na<br><br>semi mbalimbali | watafanya mazoezi ya kutambulishana<br><br>mshiriki atafanya mazoezi ya kuandika na kuzungumza<br><br>mshiriki atasalimiana na wenyeji baada ya kujifunza maarifa mapya (mbinu za kusalimiana) | | utamaduni wa Mtanzania? | |
| **Familia** | Kuweza kutambulisha ndugu na uhusiano wao katika familia | Kitenzi *kuwa na* wakati uliopo, uyakinishi na ukanushi<br><br>Namba 1 hadi 9 na upatanishi wao wa kisarufi<br><br>Ngeli ya M-/Wa- na A-/WA- | Msamiati unaolandana na maudhui na muktadha wa familia – Nomino<br><br>Vitenzi na<br><br>Semi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha viwakilishi nafsi, kitenzi *kuwa na* na utaifa<br><br>Mshiriki katika jozi atafanya mazoezi ya kutambulisha familia yake<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika<br><br>Mshiriki atatumia ujuzi wao kuwasiliana na wenyeji wao | Majadiliano, Igizodhima, Picha, Nyimbo, kadi | Je, mshiriki aliweza kuwatambulisha ndugu na kutaja uhusiano wake?<br><br>Je, ameweza kuzingatia utamaduni katika kutambulishana?<br><br>Je, ameweza kulinganisha na kutofautisha utambulisho kwa kuzingatia utamaduni? | 6 |
| **Hotelini** | Kuweza kuagiza vyakula na vinywaji | Kitenzi kuna – uyakinishi na ukanushi<br><br>‘na’ baada ya | Msamiati unaolandana na muktadha wa hotelini – | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha uagizaji wa vyakula na vinywaji hotelini<br><br>akiwa katika vikundi /jozi kila | Majadiliano, Picha, Igizodhima, | Je, mshiriki ameweza kuagiza mahitaji yake hotelini? | 6 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kiambishi tamati -je<br><br>Namba kuanzia 10 hadi 10,000 | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Viulizi | mshiriki atafanya mazoezi ya kuagiza chakula na vinywaji hotelini<br><br>mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu kupata mahitaji yake hotelini<br><br>Kila mshiriki ataigiza ununuzi wa mahitaji hotelini<br><br>Mshiriki atatumia ujuzi alioupata kuagiza mahitaji yake hotelini | | | |
| **Dukani** | Kuweza kuuliza bei za vitu na kuvinunua | Njeo iliyopita na ijayo timilifu<br><br>Wakati uliopita na ujao kanushi<br><br>Viwakilishi onyeshi | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Semi<br><br>Rangi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kuuliza bei na kununua vitu kutoka dukani<br><br>akiwa katika vikundi /jozi mshiriki atafanya mazoezi ya kuuliza na kununua vitu kutoka dukani<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu kuuliza na kununua vitu dukani<br><br>Mshiriki atauliza na kununua mahitaji yao dukani<br><br>Mshiriki atatumia ujuzi alioupata kuuliza na kununua mahitaji yao dukani na kuomba kupunguziwa bei | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video, igizodhima | Je, mshiriki ameweza kununua mahitaji yake dukani?<br><br>Je, ameweza kuomba punguzo la bei na kununua mahitaji yake? | 5 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |
| **Sokoni** | Kuweza kupatana bei na kununua matunda, mboga na vyakula | Njeo timilifu yakinishi -me- na -ja- kanushi<br><br>Njeo zote nne – wakati uliopo, uliopita timilifu, uliopita na ujao (yakinishi na kanushi) | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Vivumishi vya sifa<br><br>Semi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kupatana bei na kununua vitu sokoni<br><br>Katika vikundi /jozi mshiriki atafanya mazoezi ya kupatana na kununua vitu sokoni<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu kupatana na kununua vitu sokoni<br><br>Mshiriki atapatana na kununua mahitaji yake sokoni<br><br>Mshiriki atatumia ujuzi alioupata kupatana na kununua mahitaji yake sokoni | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video, kadi za bei, igizodhima | Je, mshiriki ameweza kununua mahitaji yake sokoni?<br><br>Je, ameweza kuomba punguzo la bei na kununua mahitaji yake? | 5 |
| **Hospitalini** | Kuweza kueleza matatizo ya afya na kupokea maelekezo ya daktari | Viambishi yambwa -ji-<br><br>Kiambishi yambwa nafsi<br><br>Kauli ya kutendwa | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Vivumishi vya sifa<br><br>Viulizi<br><br>Semi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kueleza masuala ya hospitali<br><br>Katika vikundi /jozi mshiriki atafanya igizodhima la hospitalini<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu masuala ya hospitalini | Picha, majadiliano, kanda za sauti na video, igizodhima, kadi | Je, mshiriki ameweza kueleza ugonjwa unaomsumbua?<br><br>Mshiriki aweze kulinganisha na kutofautisha huduma ya afya za hapa na za sehemu anazotoka | 6 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mshiriki atatumia ujuzi alioupata kujieleza hospitalini | | | |
| **Shughuli za kila siku** | Kuweza kueleza shughuli za kila siku | Njeo ya mazoea Hu-<br><br>Saa kwa Kiswahili<br><br>Kionyeshi -ni | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Mahali<br><br>Siku za wiki<br><br>Semi<br><br>Msamiati wa saa | Mkufunzi atatumia mbinu ya mawasiliano kujadiliana kuhusu shughuli za kila siku<br><br>Mkufunzi ataongoza majadiliano kuhusu shughuli za kila siku<br><br>Katika jozi/vikundi mshiriki atajadili kuhusu shughuli zake za kila siku<br><br>Mshiriki atajadili masuala ya jinsia katika shughuli za kila siku za hapa Tanzania na za nchi anakotoka<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuandika na kuzungumza | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video, igizodhiadi | Je, mshiriki ameweza kuelezea kuhusu shughuli zao za kila siku?<br><br>,Ameweza kutofautisha kati ya majukumu ya wanawake na wanaume? | 6 |
| **Ofisini** | Kuweza kueleza shughuli na taratibu za ofisini | Kitenzi *Kuwa na* - yakinishi – njeo za wakati uliopo, ujao, uliopita na timilifu<br><br>Kanushi – njeo zote nne | Nomino<br><br>Vifupisho<br><br>Vitenzi<br><br>Semi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha shughuli za ofisini<br><br>Katika vikundi /jozi mshiriki atazungumzia kuhusu shughuli za ofisini<br><br>Mshiriki atalinganisha na kutofautisha shughuli za ofisini mwakeo | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video, igizodhima, kadi | Je, mshiriki ameweza kuzungumzia kuhusu shughuli na taratibu za ofisi?<br><br>Je, mshiriki ameweza kulinganisha shughuli na taratibu za kiofisi yeye na wenzake ? | 6 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika | | | |
| **Usafiri na Safari** | Kuweza kuuliza na kupokea maelezo au maelekezo ya usafiri | -po- ya wakati<br><br>kitenzi ku- | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Vielezi<br><br>Pande za dira<br><br>Semi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kuhusu kuuliza na kupokea maelezo na maelekezo ya usafiri<br><br>Katika vikundi /jozi mshiriki atafanya mazoezi ya kuuliza na kupokea maelekezo ya usafiri<br><br>Mshiriki atalinganisha njia mbalimbali za usafiri zinazopatikana hapa Tanzania na nchini kwake<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu kuuliza na kupokea maelekezo ya usafiri<br><br>Mshiriki atatumia ujuzi alioupata kuuliza na kupokea maelekezo ya usafiri | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video, kadi, igizodhima | Je, mshiriki ameweza kupokea na kufuata maelekezo ya usafiri?<br><br>Je, mshiriki ameweza kutofautisha njia mbalimbali za usafiri? | 4 |
| **Utalii** | Kuweza kueleza kuhusu wanyama<br><br>Kuweza kuzungumzia vivutio vya | Viambishi vya uonyeshi –ko- -po-, -mo – yakinishi na kanushi<br><br>Kauli rai | Nomino<br><br>Majina ya wanyama<br><br>Vitenzi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kuhusu wanyama  na vivutio mbalimbali vya utalii vinavyopatikana nchini Tanzania<br><br>akiwa katika vikundi /jozi mshiriki | Picha, ramani ya Tanzania, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na | Je, mshiriki ameweza kuzungumzia kuhusu wanyama mbalimbali aliowaona mbugani? | 6 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | utalii | kanushi<br><br>Upatanisho wa vivumishi –ote-, -o-ote na -ingine | Semi | atajadili vivutio vya utalii na wanyama wanaopatikana nchini Tanzania<br><br>Mshiriki atalinganisha wanyama na vivutio mbalimbali vinavyopatikana hapa Tanzania na nchini kwake<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu wanyama na vivutio vinavyopatikana Tanzania | video, igizodhima, kadi | Je, mshiriki ameweza kutofautisha kati ya mbuga na hifadhi?<br><br>Je, mshiriki ameweza kuzungumzia kuhusu vivutio vinavyopatikana nchini Tanzania? | |
| **Hali ya hewa na majira** | Kuweza kueleza hali ya hewa, majira na shughuli mbalimbali | Ngeli ya N-/N-<br><br>Ngeli ya Ji-/ Ma-<br><br>Ngeli ya Mu-/Mi- | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Semi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kuhusu hali ya hewa, majira na shughuli mbalimbali<br><br>akiwa katika vikundi /jozi mshiriki atafanya mazoezi ya kueleza hali ya hewa, majira na shughuli mbalimbali<br><br>Mshiriki atalinganisha hali ya hewa, majira na shughuli mbalimbali zinazofanyika<br>hapa Tanzania na nchini kwake<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu hali ya hewa, majira na shughuli mbalimbali zinazofanyika katika | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video, igizodhima, kadi | Je, mshiriki ameweza kueleza kuhusu hali ya hewa nchini Tanzania?<br><br>Je, ameweza kuzungumzia kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanyika kwa kuzingatia hali ya hewa na majira mbalimbali?<br><br>Je, ameweza kutofautisha majira ya Tanzania na ya huko anakotoka? | 6 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | majira hayo<br><br>Mshiriki atatumia ujuzi alioupata kuzungumzia kuhusu hali ya hewa, majira na shughuli mbalimbali | | | |
| **Barua kwa rafiki** | Kuweza kuwasiliana kwa barua | -ki- ya masharti/kama na ikiwa – yakinishi na kanushi<br><br>Vilinganishi | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Semi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kuhusu kuwasiliana kwa barua<br><br>akiwa katika vikundi /jozi mshiriki atafanya mazoezi ya kuwasiliana kwa barua<br><br>Mshiriki atalinganisha njia mbalimbali zinazotumika katika mawasiliano<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu kuwasiliana kwa barua<br><br>Mshiriki atatumia ujuzi alioupata kuandika barua | Majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video, igizodhima, barua | Je, mshiriki ameweza kuandika barua kwa rafiki zake? | 4 |
| **Nyumba yangu** | Kuweza kueleza mazingira ya ndani na nje ya nyumba | Ngeli ya Ki-/Vi- (na Ch-/Vy-) | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Semi<br><br>Vihisishi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kuhusu kuelezea mazingira ya ndani na nje ya nyumba<br><br>akiwa katika vikundi /jozi mshiriki atafanya mazoezi ya kueleza | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video, igizodhima | Je, mshiriki ameweza kuelezea mazingira ya ndani na nje kwa ufasaha?<br><br>Je, mshiriki ameweza | 6 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Vielezi vya mahali<br><br>Vivumishi | mazingira ya ndani na ya nje ya nyumba<br><br>Mshiriki atalinganisha nyumba zinazopatikana hapa Tanzania na nchini kwake<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu mazingira ya ndani na nje ya nyumba<br><br>Mshiriki atatumia ujuzi alioupata kuelezea mazingira ya ndani na nje ya nyumba | | kutofautisha nyumba zilizoko nchini Tanzania na huko anakotoka? | |
| **Kupika** | Kuweza kueleza namna ya mapishi ya vyakula mbalimbali | Ngeli ya U-/N-<br><br>Vitenzi virudufu<br><br>Kiunganishi 'ili' | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Vitenzi vya kurudiarudia<br><br>Vielezi<br><br>Semi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kuhusu namna ya kupika vyakula mbalimbali<br><br>akiwa katika vikundi /jozi mshiriki atafanya mazoezi ya kupika chakula anachokipenda<br><br>Mshiriki atalinganisha njia mbalimbali za kupika zinazotumiwa hapa Tanzania na nchini kwake<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu kupika chakula anachokipenda | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video, igizodhima, kadi | Je, mshiriki ameweza kuandaa vyakula mbalimbali kwa kuzingatia njia za upishi zilizobainishwa? | 4 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mshiriki atatumia ujuzi alioupata kupika chakula anachokipenda | | | |
| **Sikukuu mbalimbali** | Kuweza kuzungumzia kuhusu sikukuu mbalimbali za kitaifa , kidini na za kijadi<br><br>Kulinganisha sikukuu za nchini kwao na za Tanzania | Kauli tendwa –w- | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Vielezi<br><br>Semi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kuhusu sikukuu mbalimbali za kitaifa, kidini na kijadi<br><br>akiwa katika kikundi /jozi mshiriki atazungumzia kuhusu sikukuu mbalimbali nchini Tanzania<br><br>Mshiriki atalinganisha sikukuu mbalimbali zinazoadhimishwa hapa Tanzania na nchini kwake<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu sikukuu zinazoadhimishwa nchini Tanzania | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video, kalenda, igizodhima, kadi za mialiko, | Je, mshiriki ameweza kuzungumzia kuhusu sikukuu mbalimbali zinazoadhimishwa nchini Tanzania?<br><br>Je, mshiriki ameweza kulinganisha sikukuu zinazoadhimishwa nchini kwao na zile zinazoadhimishwa hapa Tanzania? | 6 |
| **Kutafuta mfanyakazi wa nyumbani** | Kuweza kupata taarifa kuhusu kuajiri mfanyakazi wa nyumbani | Matumizi mbalimbali ya kitenzi elekezi piga<br><br>Matumizi mbalimbali ya neno<br><br>Matumizi ya maneno | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Vivumishi<br><br>Semi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kuhusu kutafuta mfanyakazi wa nyumbani<br><br>akiwa katika vikundi /jozi mshiriki atafanya mazoezi ya kutafuta mfanyakazi wa nyumbani<br><br>Mshiriki atalinganisha njia mbalimbali zinazotumika kumpata mfanyakazi wa nyumbani na ubora | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video | Je, mshiriki ameweza kupata mfanyakazi wa ndani baada ya kufuata hatua zote muhimu?<br><br>Je, ameweza kutofautisha upatikanaji wa mfanyakazi wa | 4 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | umuhimu, shuruti, pendekezo na rai | | au hatari zake<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu kupata mfanyakazi wa nyumbani | | nyumbani kati ya Tanzania na nchi anakotoka? | |
| **Hotelini** | Kuweza kuuliza bei za chumba hotelini na kupokea maelekezo ya huduma mbalimbali hotelini | -enye | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Semi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kuhusu kupata chumba hotelini<br><br>akiwa katika vikundi /jozi kila mshiriki atafanya mazoezi ya kuuliza bei ya chumba na huduma mbalimbali hotelini<br><br>Mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu namna ya kupata vyumba hotelini<br><br>Mshiriki atatumia ujuzi alioupata kuweza kuulizia vyumba na huduma nyingine hotelini | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video, igizodhima, kadi | Je, mshiriki amefanikiwa kupata chumba hotelini?<br><br>Je, mshiriki amezingatia maelekezo yaliyotolewa na wahudumu wa hotelini? | 4 |
| **Ajali barabarani** | Kuweza kueleza kuhusu tukio la ajali yoyote ya barabarani | -ka- ya masimulizi | Nomino<br><br>Vitenzi<br><br>Vivumishi<br><br>Semi | Mkufunzi atatumia mbinu ya *mawasiliano* kufundisha kuhusu kueleza tukio la ajali barabarani<br><br>Akiwa katika vikundi /jozi kila mshiriki atafanya mazoezi ya kuripoti ajali ya barabarani<br><br>Mshiriki atalinganisha matukio ya | Picha, majadiliano, nyimbo, kanda za sauti na video, kadi, igizodhima | Je, mshiriki ameweza kuelezea ajali yoyote aliyoiona?<br><br>Je mshiriki ameweza kuonyesha tofauti yoyote ya kushughulikia ajali | 4 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ajali za barabarani hapa Tanzania na nchini kwao<br><br>Kila mshiriki atafanya mazoezi ya kuzungumza na kuandika kuhusu ajali barabarani<br><br>Mshiriki atatumia ujuzi alioupata kutoa taarifa ya ajali | | kati ya Tanzania na nchi zingine? Ametoa sababu gani? | |

**MAREJEO**


BAKITA (2014) *Furahia Kiswahili: Kiswahili kwa Wageni Hatua ya Kwanza.* Dar es Salaam. Baraza la Kiswahili la Taifa

BAKIZA () *Mawasiliano ya Msingi: Kiswahili kwa Wageni*. Dar es Salaam. Educational Books Publishers

Russel, J. (2003) *Teach Yourself Swahili*. London. The McGraw-Hill Companies

Senkoro, F.E.M.K (2003) Tuseme *Kiswahili: A Multdimensional Approach to Teaching and Learning of Swahili as a Foreign Language*. Madison, National African Language Resource Center

SUZA (2013) *Zungumza Kiswahili: Hatua ya Kwanza*. Dar es Salaam, Educational Books Publishers LTD.

TUKI, (1997) *Sema Kiswahili: Furahia Tanzania*, Dar es Salaam. (Unpublished)

Wilson, M. P. (2010) *Simplified Swahili*. Edinburgh. Pearson Educational Limited